

MKATABA WA KUPANGISHA ARDHI

MKATABA HUU wa upangishaji umefanyika na kuingiwa tarehe 21/06/2025

kati ya:

ROMBO MEIBUKO wa Kindasikira, Mererani, Simanjiro (hapa atajulikana kama

'MPANGISHAJI')

NA

H & S MINERALS LIMITED ya S.L.P. 218, Shinyanga (hapa itajulikana kama

'MPANGAJI').

WOTE KWA PAMOJA wanakubaliana yafuatayo:

KUSUDI LA MKATABA

Mpangishaji anakubali kumpangisha Mpangaji eneo la ardhi lenye ukubwa wa ekari tano (5) lililopo karibu na Ofisi Mpya za Madnii, Mererani, Simanjiro kwa ajili ya kujenga na kuendesha kituo cha kuchakata madini.

MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utadumu kwa muda wa miaka mitatu (3) kuanzia tarehe ya kusainiwa kwake, na unaweza kurekebishwa au kuhuishwa kwa makubaliano ya maandishi ya pande zote mbili.

MALIPO YA KODI

Mpangaji atailipa Mpangishaji kodi ya pango ambayo ni shlingi za kitanzania milioni nne na laki tano (4,500,000) na kulipwa kwa wakati kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba huu.

HAKI NA WAJIBU WA MPANGISHAJI

- a) Kumpa Mpangaji ruhusa ya kutumia eneo bila bughudha.
- b) Kuhakikisha kuwa eneo hilo ni mali yake halali na halina mgogoro.
- c) Kumsaidia Mpangaji kupata usaidizi wowote wa kisheria au kijamii unaohitajika.

HAKI NA WAJIBU WA MPANGAJI

- a) Kutumia eneo kwa madhumuni yaliyokubaliwa tu.
- b) Kulinda na kuheshimu mipaka ya eneo.
- c) Kulipa kodi ya pango kwa wakati kama ilivyokubaliwa.

UVUNJWAJI WA MKATABA

Iwapo upande wowote utashindwa kutimiza masharti ya mkataba huu, upande mwingine utakuwa na haki ya kuvunja mkataba kwa kutoa taarifa ya maandishi ya siku thelathini (30).

SHERIA INAYOTUMIKA

Mkataba huu unasimamiwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA USHAHIDI WAWOTE HAPO JUU, pande zote mbili zimetia saini mkataba huu tarehe 21/06/2025.

Imetiwa saini mbele yangu na

.....**ROMBO MEIBUKO**.....ambaye

Namfahamu/alietambulishwa kwangu na

.....ambaye namfahamu


Leo tarehe 21/06/2025.

Jina: **ANNA TUMAINI MWITA**.....

Sahihi:

Tarehe: 21/06/2025



}
..........
MPANGISHAJI

Wadhifa: ...WAKILI.....

MPANGAJI:

Kwa niaba ya H & S MINERALS LIMITED

Jina: ...HILAL SOUD AHMED.....

Cheo: ...MKURUGENZI.....

Sahihi: ...H.Ahmed.....

Tarehe: 21/06/2025

Imetiwa saina mbele yangu na

...HILAL SOUD AHMED.....ambaye

Namfahamu/alietambulishwa kwangu na

.....-.....ambaye namfahamu

Leo tarehe: 21/06//2025.

Jina: ...ANNA TUMAINI MWITA.....

Sahihi: ...Anna.....

Tarehe: 21/06/2025

Wadhifa: ...WAKILI.....



}
...H.Ahmed.....
MPANGAJI